



NISHATI

HABARI ZA
NISHATI

News *Bulletin*



www.nishati.go.tz



Wizara ya Nishati



wizara_ya_nishati_tanzania



@Nishati2017




Wizara ya Nishati

Toleo Namba 21

Disemba 1-31, 2020

RAIS ALIELEZA BUNGE VIPAUMBELE SEKTA YA NISHATI

UK.
7



UK.
2

Waziri Mkuu azindua uchepushwaji wa maji katika mradi wa JNHPP



LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA
MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au
Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P 2494, Dodoma

RAIS ALIELEZA BUNGE VIPAUMBELE SEKTA YA NISHATI

Hafsa Omar - Dodoma

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt John Pombe Magufuli amesainisha vipaumbele katika sekta ya nishati kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, chini ya serikali aliyopewa dhamana kuiongoza kwa awamu nyingine ya pili.

Akilihutubia Bunge la 12 wakati akilizindua jijini Dodoma, Novemba 13 mwaka huu, Rais Magufuli alieleza kuwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali yake imejipanga kufikisha umeme kwenye vijiji vyote ambavyo bado havijafikishiwa nishati hiyo ambavyo alivitaja kuwa havizidi 2,384.

“Takwimu za hadi jana zinaonesha tumefikisha umeme kwenye vijiji 9,884 kutoka vijiji 2,018 mwaka 2016. Nchi yetu ina jumla ya vijiji 12,280,” alifafanua.

Aidha, Rais alieleza kipaumbele kingine kuwa ni kuimarisha miundombinu ya nishati na kuboresha upatikanaji wa huduma za umeme nchini.

Akifafanua, alisema kuwa katika kutekeleza hilo, Serikali yake inakusudia kukamilisha ujenzi wa Bwawa la kufua umeme la Nyerere, litakalozalisha megawati 2,115 sambamba na kuanza ujenzi wa miradi mingine mipya ya umeme wa maji katika maeneo mbalimbali.

Aliitaja miradi hiyo kuwa ni pamoja na

utakaotekelezwa katika eneo la Luhudji (megawati 358), Lumakali (megawati 222), Kikonge (megawati 300).

Mingine ni ya umeme wa gesi asilia Mtwara (megawati 300), Somanga Fungu (megawati 330), Kinyerezi III (megawati 600), Kinyerezi IV (megawati 300) pamoja na miradi mingine midogo midogo.

Vilevile, Rais alibainisha kuwa makusudio mengine ya Serikali ni kuzalisha umeme megawati 1,100 kwa kutumia nishati jadidifu yaani jua, upepo na joto ardhi.

Aliendelea kueleza kuwa katika kipindi hicho, Serikali yake imepanga kukamilisha mradi wa kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 400 kutoka Singida - Arusha

hadi Namanga pamoja na unaoanzia Iringa - Mbeya hadi Tunduma ambayo alisema itaiunganisha Tanzania na nchi jirani za Kenya na Zambia.

Kuhusu maeneo ambayo hayaunganishwa katika gridi ya Taifa, Rais Magufuli alisema Serikali imepanga kuyaunga maeneo muhimu ya nchi ikiwemo Kigoma.


Aliongeza kuwa, katika kipindi kilichopita cha uongozi wake, Serikali ilitekeleza miradi mingi ya kusafirisha umeme na hivyo kupunguza matumizi ya umeme wa mafuta hatua iliyowezesha kuokoa kiasi cha shilingi bilioni 719 kwa mwaka.

“Miradi hii yote ya umeme itakapokamilika, siyo tu itatuwezesha kuwa na umeme wa kutosha na kuufikisha kwenye maeneo yote nchini, bali

pia itatuwezesha tuwe na ziada ya kuweza kuuza nje. Pia, itasaidia kupungua kwa gharama za umeme.”

Akizungumzia sekta ndogo ya mafuta na gesi, Rais Magufuli alisema kuwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali itaanza utekelezaji wa miradi ya kielelezo ya bomba la mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Bandari ya Tanga.

Aidha, alieleza kipaumbele kingine kuwa ni kuhakikisha mradi wa kusindika gesi mkoani Lindi, unaanza sambamba na kuhamasisha matumizi ya gesi asilia na gesi ya mitungi majumbani, kwenye taasisi, viwanda na magari ili kupunguza uharibifu wa mazingira na athari za mabadiliko ya tabia nchi.





BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti

Mhandisi Zena Said
(Katibu Mkuu)

Makamu Mwenyekiti

Mhandisi Leonard Masanja
(Naibu Katibu Mkuu)

Mhariri

Dorina G. Makaya

Waandishi

Teresia Mhagama
Zuena Msuya
Hafsa Omar

Msanifu Kurasa

Lucas Gordon

Wasiliana nasi kwa simu
namba +255-26-2322018
Nukushi: +255-26-2320148
au

Fika Ofisi ya Mawasiliano
Mitumba Dodoma,
S.L.P 2494, Dodoma



www.nishati.go.tz



Wizara ya Nishati



@Nishati2017



wizara_ya_nishati_tanzania



Wizara ya Nishati

VIPAUMBELE SEKTA YA NISHATI VITAIMARISHA UPATIKANAJI WA NISHATI NCHINI

Kila mtu anafahamu umuhimu wa Nishati katika kuleta maendeleo ya nchi, yawe ya kiuchumi au kijamii kwani nishati huchochea uwepo wa shughuli mbalimbali za kiuchumi kama vile uanzishaji wa viwanda vikubwa na vidogo pamoja na kuboresha huduma za kijamii kama vile upatikanaji wa huduma bora za maji, afya na elimu.

Kwa kutambua umuhimu wa nishati nchini, Serikali imekuwa ikijikita katika kuendeleza na kusimamia ipasavyo miradi mbalimbali ya nishati kama ya Gesi Asilia na umeme lengo likiwa ni kufikisha nishati husika katika kila eneo nchini ili wananchi waweze kuitumia kujiletea maendeleo.

Akizindua Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, jijini Dodoma, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt John Pombe Magufuli aliainisha vipaumbele katika sekta ya nishati kwa kipindi cha mwaka 2020-2025 ambavyo kila mhusika akivifanyia kazi, vitazidi kuboresha hali ya upatikanaji wa nishati nchini.

Moja ya Vipaumbele vilivyotajwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt John Pombe Magufuli, ni kufikisha umeme kwenye vijiji vyote ambavyo bado havijafikishiwa nishati hiyo ambavyo alisema kuwa havizidi 2,384.

Katika usambazaji wa umeme vijijini alieleza kuwa, takwimu za hadi tarehe 12 Novemba, 2020 zinaonesha umeme umefikishwa kwenye vijiji 9,884 kutoka vijiji 2,018 mwaka 2016.

Kipaumbele kingine cha Serikali, alisema ni kuimarisha miundombinu ya nishati na kuboresha upatikanaji wa huduma za umeme nchini ambapo Serikali inakusudia kukamilisha ujenzi wa Bwawa la kufua umeme la Julius Nyerere, litakalozalisha megawati 2,115 sambamba na kuanza ujenzi wa miradi mingine mipya ya umeme wa maji katika maeneo mbalimbali.

Aliitaja miradi hiyo kuwa ni pamoja na utakaotekelezwa katika eneo la Luhudji (megawati 358), Lumakali (megawati 222), Kikonge (megawati 300).

Aidha, katika Gesi Asilia alisema kuwa Serikali inakusudia kutekeleza miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia Gesi asilia ya Mtwara (megawati 300), Somanga Fungu (megawati 330), Kinyerezi III (megawati 600), Kinyerezi IV (megawati 300) pamoja na miradi mingine midogo

midogo.

Katika Nishati Jadidifu, Mhe. Dkt John Pombe Magufuli, alisema kuwa, makusudio ni kuzalisha umeme wa megawati 1,100 kwa kutumia vyanzo vya Jua, Upepo na Jotoardhi.

Kuhusu maeneo ambayo hayajaunganishwa na umeme wa gridi ya Taifa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Magufuli alisema kuwa Serikali imepanga kuyaunga maeneo hayo na umeme wa Gridi ya Taifa ambao hupelekea kuokoa fedha nyingi ambazo zingetumika katika kununua mafuta ya kuzalishia umeme.

Katika miradi ya kusafirisha umeme alieleza kuwa, kipaumbele ni kutekeleza miradi ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 400 kutoka Singida – Arusha hadi Namanga pamoja na unaoanzia Iringa – Mbeya hadi Tunduma ambayo itaiunganisha Tanzania na nchi jirani za Kenya na Zambia.

Akizungumzia sekta ndogo ya Mafuta na Gesi, Rais Magufuli alisema kuwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali itaanza utekelezaji wa miradi ya kielelezo ya Bomba la Mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Bandari ya Tanga.

Aidha, alitaja kipaumbele kingine kuwa ni kuhakikisha mradi wa kusindika Gesi mkoani Lindi, unanza sambamba na kuhamasisha matumizi ya Gesi Asilia na Gesi ya mitungi majumbani, kwenye taasisi, viwanda na magari ili kupunguza uharibifu wa mazingira na athari za mabadiliko ya tabia nchi.

Kwa vipaumbele hivi vilivyoainishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli, vinaonesha wazi kuwa, mara vitakapotekelezwa vitawezesha nchi kuwa na nishati ya kutosha na ya uhakika kuweza kufikishwa katika maeneo yote nchini na hivyo kuwawezesha wananchi kutumia nishati hii katika shughuli za kimaendeleo na hivyo kuongeza pato la mwananchi mmoja mmoja na nchi kwa ujumla.

Tunatoa wito kwa wataalam wote kuweza kufanya kazi kwa weledi ili kuhakikisha kuwa vipaumbele hivi vilivyoainishwa na Rais wa nchi, vinatekelezwa kwa ufanisi na ndani ya muda uliopangwa ili nishati iweze kuchochea zaidi maendeleo ya nchi.

Waziri Mkuu azindua uchepushwaji wa maji katika mradi wa JNHPP

Na Zuena Msuya, Pwani

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa amezindua njia ya mchepuko ya kupitisha maji kwenye mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) ili kuruhusu ujenzi wa tuta kuu la kuzuia maji ya bwawa yatakayozalisha umeme.

Uzinduzi huo ulifanyika tarehe 18 Novemba, 2020, katika eneo la Mradi, Rufiji mkoani Pwani na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwemo wanaohusika na Sekta ya Nishati katika nchi za Tanzania na Misri.

Katika uzinduzi huo, Waziri Mkuu Mhe. Majaliwa alisema kuwa, mradi huo utakaozalisha megawati 2100 ni mkubwa, wa kimkakati na aina yake katika ukanda wa Afrika ambapo unashika nafasi ya nne kwa ukubwa, pia ni wa kwanza kwa Afrika Mashariki na Kusini.

Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa alieleza



Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa (wa pili kushoto), Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said (kushoto) na aliyekuwa Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (pili kulia) wakielekea eneo la kuzindua uchepushaji wa maji ya mto Rufiji kupitia handaki ili kuruhusu ujenzi wa tuta kubwa la kuzuia maji ya bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere (JNHPP), Novemba 18, 2020, mkoani Pwani.

INAENDELEA UK.

5



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (wa pili kushoto), Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said (wa pili kulia) na aliyekuwa Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (kulia) wakibonyeza kitufe kuashiria uzinduzi wa uchepushaji wa maji ya mto Rufiji kupitia handaki ili kuruhusu ujenzi wa tuta kubwa la kuzuia maji ya bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere (JNHPP), Novemba 18, 2020, mkoani Pwani.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (wa pili kushoto), Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said (wa pili kulia) na aliyekuwa Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (kulia) wakibonyeza kitufe kuashiria uzinduzi wa uchepushaji wa maji ya mto Rufiji kupitia handaki ili kuruhusu ujenzi wa tuta kubwa la kuzuia maji ya bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere (JNHPP), Novemba 18, 2020, mkoani Pwani.

Waziri Mkuu azindua uchapushwaji wa maji katika mradi wa JNHPP



Mhandisi Mkazi ambaye pia ni mshauri wa mradi wa JNHPP, Mhandisi Mushubila Kamuhabwa (kulia) akimuonesha Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa (katikati), eneo ambalo maji ya mto yanachepushwa kupitia handaki ili kuruhusu ujenzi wa tuta kubwa la bwawa la maji ya kuzalisha umeme. Kushoto ni Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said.

kwa hatua iliyofika mpaka sasa.” alisema Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa..

“Aidha, natoa wito kwa wataalam wetu wa ndani kutumia fursa hii ya kujengewa uwezo, kujifunza kila wanachokifanya wataalam kutoka nje ili waje kusaidia katika miradi mingine.” alisisitiza Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa.

Kuhusu utekelezaji wa mradi huo, alisema kuwa ameridhishwa na kasi ya ujenzi wa mradi huo wa bwawa la kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Bonde la Mto Rufiji.

Pia, aliipongeza Wizara ya Nishati pamoja na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa hatua waliyofikia katika ujenzi wa bwawa hilo na kuwataka kuongeza kasi ili kukamilisha mradi huo ndani ya muda uliopangwa au hata kabla ya muda huo.

Vilevile aliwasisitiza wasimamizi wa mradi huo kufanya kazi zao kwa weledi, uzalendo

INATOKA UK.

4

kuwa, Serikali imekuwa mstari wa mbele kuhakikisha ujenzi wa mradi huo unatekelezeka kwa wakati kwani utapelekea kuwepo kwa umeme mwingi, wa kutosha na wa gharama nafuu utakaoboresha hali ya uchumi wa nchi na wananchi.

Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa Aliongeza kuwa, mradi huo utakapokamilika utawezesha taifa kuongeza mapato yake kwa kuongeza shughuli za kiuchumi, pia kufanya biashara ya umeme kwa nchi jirani na zenye uhitaji na pia umeme

huo utatumika katika viwanda nchini.

Pia aliweka wazi kuwa, Serikali inaugharamia mradi huo kwa asilimia 100 na hadi sasa tayari mkandarasi ameshalipwa shilingi Trilioni 1.57 kulingana na kazi zilizofanyika, na mradi huo unatarajiwa kugharimu shilingi Trilioni 6.55 hadi kukamilika kwake.

“Nawahakikishia Watanzania tujivunie kwa kuwa na mradi huu, tutembe kufua mbele kwa kuweza kutekeleza mradi huu wa JNHPP, nawahakikishia kuwa mahusiano kati yetu na makampuni yanayotekeleza mradi ni mazuri, hatuna deni lolote

INAENDELEA UK.

6



Mhandisi Mkazi ambaye pia ni mshauri wa mradi wa JNHPP, Mhandisi Mushubila Kamuhabwa (kulia) akitoa maelezo kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (pili kulia), wakati akiwasili eneo la ujenzi wa mradi wa Julius Nyerere ili kuzindua uchapushaji wa maji ya mto Rufiji kupitia handaki ili kuruhusu ujenzi wa tuta kuu. Kushoto ni Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said, na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Dkt. Tito Mwinuka (kulia).

Waziri Mkuu azindua uchepushwaji wa maji katika mradi wa JNHPP



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (katikati) akiandika jambo baada ya kuzindua uchepushaji wa maji ya mto Rufiji kupitia handaki ili kuruhusu ujenzi wa tuta kuu. Kulia ni Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said.



Aliyekuwa Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akizungumza na wageni waliohudhuria uzinduzi wa uchepushaji wa maji ya mto Rufiji kupitia handaki ili kuruhusu ujenzi wa tuta kuu katika mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP).

INATOKA UK.

5

na kuweka mbele maslahi ya taifa na kwamba wahakikishe makubaliano ya kutekeleza miradi ya kijamii kama ilivyoelekezwa katika mkataba yanatekelezwa.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said alisema kuwa utekelezaji wa mradi huo utaenda sambasamba na utekelezaji wa miradi ya kijamii katika vijiji vilivyo karibu, katika mkoa wa Pwani na Morogoro kwa lengo la kujenga mahusiano mazuri na wananchi.

Mhandisi Said alisema tayari mradi huo umeshatoa ajira za moja kwa moja 6,364, ambapo watanzania 5,728 wamenufaika na ajira hizo.

Aliendelea kuwa, mkandarasi atatekeleza

miradi miwili ya kijamii ambayo ni ujenzi wa barabara yenye urefu wa Kilometa 41 kutoka stesheni ya treni ya Fuga hadi katika eneo la mradi na ujenzi wa kiwanja cha kisasa cha michezo kinachotarajiwa kujengwa mkoani Dodoma.

Kwa upande wake, aliyekuwa Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani aliishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuridhia na kutoa fedha za kutekeleza ujenzi wa mradi huo bila vikwazo vyovyote hadi hapo ulipofikia huku shughuli za ujenzi zikiendelea kwa kasi inayoridhisha.

Hata hivyo aliwashauri wasimamizi na wakandarasi wanaotekeleza mradi huo kufanya kazi kwa bidii na maarifa, huku wakijua kuwa mradi huo unatekelezwa kwa manufaa ya watanzania na taifa kwa ujumla.

Aliwahamasisha wawekezaji kutumia fursa hiyo kuja kuwekeza zaidi nchini kwa kuwa kutakuwa na umeme wa kutosha, wa uhakika na gharama nafuu kuweza kuendesha shughuli za kiuchumi na pia Tanzania ina sera nzuri na bora za kuwavutia wawekezaji katika nyanja mbalimbali za kiuchumi.



Baadhi ya wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wakimsikiliza Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (hayupo pichani) wakati wa uzinduzi wa uchepushaji wa maji ya mto Rufiji kupitia handaki ili kuruhusu ujenzi wa tuta kuu katika mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP).



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza na wageni waliohudhuria uzinduzi wa uchepushaji wa maji ya mto Rufiji kupitia handaki ili kuruhusu ujenzi wa tuta kuu katika mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP). Kulia ni Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said.



Baadhi ya Viongozi Wakuu wa Wizara ya Nishati, wakibadilishana mawazo wakati wa uzinduzi wa uchepushaji wa maji ya mto Rufiji kupitia handaki ili kuruhusu ujenzi wa tuta kuu katika mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP).



Baadhi ya Viongozi wakuu wa Wizara ya Nishati, wakimsikiliza Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa wakati wa uzinduzi wa uchepushaji wa maji ya mto Rufiji kupitia handaki ili kuruhusu ujenzi wa tuta kuu katika mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP).



Baadhi ya Viongozi wakuu wa Wizara ya Nishati, (waliosimama) wakiwa katika picha ya pamoja na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (waliokaa katikati) wakati wa uzinduzi wa uchepushaji wa maji ya mto Rufiji kupitia handaki ili kuruhusu ujenzi wa tuta kuu katika mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP).



Baadhi ya wageni waliohudhuria uzinduzi wa uchepushaji wa maji ya mto Rufiji kupitia handaki ili kuruhusu ujenzi wa tuta kuu katika mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP).

NAIBU KATIBU MKUU NISHATI AMTAKA MKANDARASI WA REA RUVUMA KUONGEZA KASI



Zuena Msuya - Ruvuma

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja amewaagiza watendaji wa kampuni ya ukandarasi ya Namis Corporate Ltd, wanaotekeleza mradi wa umeme vijijini (REA), mkoani Ruvuma, kuongeza kasi ili wakamilishe kazi hiyo kwa wakati.

Alitoa maagizo hayo kwa nyakati tofauti akiwa katika ziara ya kazi iliyolenga kukagua maendeleo ya utekelezaji

INAENDELEA UK.

9

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (wa tatu - kulia), akitoa maelekezo kwa Ujumbe aliambatana nao wakati wa ziara yake iliyolenga kukagua maendeleo ya usambazaji wa umeme vijijini, wilayani Mbinga, Mkoa wa Ruvuma, Novemba 10 na 11, 2020.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (mwenye miwani), akipitia taarifa ya utekelezaji wa mradi wa usambazaji umeme vijijini, wilayani Nyasa, mkoani Ruvuma, alipokuwa katika ziara ya kazi Novemba 10 na 11, 2020.



NAIBU KATIBU MKUU NISHATI AMTAKA MKANDARASI WA REA RUVUMA KUONGEZA KASI



Mwakilishi wa kampuni ya ukandarasi ya Namis Corporate Ltd, inayotekeleza mradi wa umeme vijijini (REA), mkoani Ruvuma, Mhandisi Joseph Lipuka (kushoto), akimuonesha Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (wa pili - kushoto) na Ujumbe alioambatana nao, njia itakayopitiwa na miundombindo ya umeme katika Wilaya ya Namtumbo. Naibu Katibu Mkuu alikuwa katika ziara ya kazi kukagua maendeleo ya usambazaji umeme vijijini, Mkoa wa Ruvuma, Novemba 10 na 11, 2020.

INATOKA UK.

8

wa mradi huo mkoani Ruvuma, Novemba 10 hadi 11 mwaka huu.

Mhandisi Masanja alimtaka mkandarasi huyo kufanya kazi kwa ubunifu na viwango huku akiiga mifano ya kampuni nyingine za ukandarasi ambazo zinafanya kazi nzuri.

Akifafanua kuhusu ubunifu, Naibu Katibu Mkuu alimwelekeza mkandarasi huyo ambaye utendaji kazi wake unasuasua, kuazima vifaa kutoka kampuni nyingine za ukandarasi au Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) badala ya

kutumia muda mrefu akisubiri vifaa alivyoagiza nje ya nchi.

“Azimeni vifaa mnavyovihitaji kutoka kwa wenzenu ili muendeleo na kazi na mtawarudishia vifaa hivyo pindi mlivyoagiza vitakapofika. Nasisitiza kuwa hakuna sababu ya msingi inayosababisha mradi kutotekelezwa kwa wakati,” alisisitiza.

Aidha, alimtaka mkandarasi husika kuongeza nguvu kazi pamoja na kulipa stahili za wafanyakazi na vibarua kwa wakati hali ambayo

alisema itaongeza morari yao ya utendaji kazi na hivyo kuwezesha kazi kukamilika kwa wakati na viwango stahiki.

Katika ziara hiyo, Naibu Katibu Mkuu aliambatana na Mwakilishi wa Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu kutoka Wizara ya Nishati, Mhandisi Christopher Bitesigirwe, Mkurugenzi wa Huduma za Ufundi kutoka Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Jones Olotu pamoja na viongozi kadhaa wa TANESCO mkoani Ruvuma.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (kushoto), akitoa maagizo kwa ujumbe alioambatana nao katika ziara yake kukagua maendeleo ya usambazaji wa umeme vijijini, wilayani Mbinga, mkoani Ruvuma, Novemba 10 na 11, 2020.

Serikali Itaendelea Kuboresha Sekta ya Nishati kwa Kasi



Na. Beatrice Saanga-MAELEZO

Nishati ni sekta muhimu sana kwa wananchi na maendeleo ya nchi kwa ujumla hususani kuelekea katika uchumi wa viwanda kwa kuhakikisha kuwa umeme wa uhakika unazalishwa na kuwafikia wananchi walio wengi ili waweze kufikia ndoto zao za kuanzisha na kumiliki viwanda na kuweza kuinuka kuinua kipato cha familia zao na kuleta maendeleo ya nchi.

Aidha, nishati ya umeme inasalia kuwa muhimu sana katika maendeleo na ukuaji wa uchumi duniani kote hasa kutokana na uhitaji mkubwa wa nishati katika matumizi ya kila siku na uzalishaji viwandani ambapo inahitajika

katika kuendesha mitambo mikubwa na katika viwanda vidogo vinavyomilikiwa na wajasiriamali wadogo.

Katika kipindi cha 2019/20, Wizara ya Nishati imekuwa na vipaumbele vingi hasa katika kuhakikisha kwamba umeme wa uhakika unapatikana ili kuwezesha ukuaji wa uchumi wa nchi ambapo Serikali inayoongozwa na Mhe. Rais John Pombe Magufuli imejitahidi kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kutekeleza miradi mikubwa ikiwemo mradi wa kuzalisha umeme katika Mto Rufiji ambao ukikamilika utakuwa na MW 2,115 uliopo wilayani Rufiji na miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia ya Kinyerezi I - Extension MW 185, Kinyerezi II MW 240, Somanga Fungu MW 330

ulioko mkoani Lindi pamoja na MW 300 ulioko katika mkoa wa Mtwara.

Aidha, Serikali imeimarisha mifumo ya usafirishaji wa umeme mkubwa nchini ikiwa ni pamoja na kuendelea na utekelezaji wa mradi wa kusambaza umeme vijijini unaosimamiwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), mradi wa ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania) na kuendelea miradi ya nishati jadidifu (jotoardhi, upepo na umeme-jua).

Jitihada za Serikali katika kuimarisha nishati zimewezesha kutekeleza miradi mingi ya kusafirisha umeme ambapo imepelekea kupunguza matumizi ya umeme wa mafuta na kuwezesha kuokoa kiasi cha shilingi bilioni, 719 kwa mwaka. Mafanikio hayo yamewezekana katika

kipindi cha miaka mitano iliyopita kuanzia 2019/20.

Wakati Tanzania inaelekea kutimiza azma ya kuwa nchi ya uchumi wa viwanda na kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa katika ya Mwaka 2025 Serikali kupitia, Wizara ya Nishati imelenga kuzalisha umeme wa MW 5,000, mwaka 2020 na kuongezeka hadi kufikia kufikisha MW 10,000 ifikapo mwaka 2025.

Mahitaji ya umeme nchini yameendelea kuongezeka kutokana na kukua kwa shughuli za kiuchumi zinazohitaji nishati ya umeme wa kutosha, wa uhakika na wenye gharama nafuu pamoja na kuimarishwa kwa mifumo ya usafirishaji na usambazaji wa umeme

Serikali Itaendelea Kuboresha Sekta ya Nishati kwa Kasi

INATOKA UK.

10

ili kupunguza tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme wa jumla ya MW 2,115 kwa kutumia maji (Hydro Power Plant) katika Bonde la Mto Rufiji ni kichocheo muhimu katika kuwezesha Tanzania kufikia azma yake ya kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025 ambapo utekelezaji wa mradi huu unategemewa kupunguza kama si kuondoa kabisa tatizo la umeme nchini

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Rais Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli itahakikisha inasimamia ipasavyo na kuimarisha miundombinu ya nishati

kwa kuhakikisha upatikanaji wa huduma za umeme unaboreshwa ili kukabiliana na changamoto mbalimbali za uimarishaji wa Mikakati ya utoaji wa huduma ya nishati ya Umeme.

Katika hotuba yake wakati akizindua Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dodoma, tarehe, 13, Novemba 2020 Mhe. Rais John Pombe Magufuli alisema Serikali yake inaenda kuwezesha upatikanaji wa umeme katika vijiji vyote ambavyo bado havijafikiwa na umeme na kuondoa kabisa tatizo la umeme vijijini.

“Kuhusu umeme pia, kwenye miaka mitano ijayo, tumepanga kufikisha umeme kwenye vijiji vyote ambavyo bado havijafikiwa umeme, ambapo idadi yake haizidi 2,384. Kwenye miaka mitano iliyopita, kwa takwimu za hadi

jana tumefikisha umeme kwenye vijiji 9,884 kutoka vijiji 12,018 mwaka 2016. Nchi yetu ina vijiji 12,280” alisema Rais Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli.

Alibainisha kuwa kwenye miaka mitano ijayo Serikali yake imejipanga kukamilisha mradi wa ujenzi wa bwawa la kufua umeme la Nyerere ambalo linategemewa kuzalisha megawati 2,115 ambapo Tanzania inakusudia kupata umeme wa kutosha kupitia mradi huo ambao unatarajiwa kupunguza bei ya umeme kwa wananchi.

Aliitaja miradi mingine ambayo Serikali inakusudia kuanza ujenzi wake katika kipindi cha miaka mitano ijayo kuwa ni pamoja na ujenzi wa miradi mingine ya umeme wa maji Ruhudji utakaokuwa na MW 358, Rumakali MW 222, Kikonge MW 300, umeme wa gesi Mtwara MW 300, Somanga Fungu MW 330, Kinyerezi

III MW 600 na Kinyerezi IV MW 300. Rais Magufuli aliongeza kuwa, Serikali pia inakusudia kutekeleza miradi mingine midogo midogo ambayo kwa pamoja inakusudiwa kuzalisha umeme MW 1,100 kwa kutumia Nishati jadidifu (jua, upepo, joto ardhi)

Katika miaka mitano ijayo Serikali itakamilisha miradi hiyo na kuwezesha upatikanaji wa umeme katika maeneo mbali mbali ya nchini, hali itakayopelekea kuimarika kwa shughuli za viwanda, kuongeza uzalishaji, pamoja na kupelekea kupanda kwa uchumi wa taifa. Pia Serikali itaendelea kuhamasisha matumizi ya gesi asilia na gesi ya mitungi majumbani, kwenye taasisi, viwanda na magari ili kupunguza uharibifu wa mazingira na athari za mabadiriko ya tabianchi.



TAARIFA MAALUM YA MAFANIKIO YA SEKTA YA NISHATI KWA KIPINDI CHA MWAKA 2015 - 2020



Kazi ya utafiti wa mafuta kwa kuchimba visima vifupi (stratigraphic boreholes) katika eneo la Eyasi Wembere kwa ajili ya kukusanya sampuli za miamba ili kutathmini uwezekano wa miamba hiyo kuhifadhi mafuta.

Katika kipindi cha mwaka 2015 – 2020, mafanikio yafuatayo yamepatikana katika sekta ya nishati:-

- Kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme nchini ambapo hadi kufikia mwaka 2020, uwezo wa mitambo ya kufua umeme nchini umeongezeka nakufikia jumla ya megawati 1,602.32 kutoka megawati 1,308 mwaka 2015. Ongezeko hili limeifanya nchi kujitosheleza kwa mahitaji ya umeme, kutokuwa na mgao wa umeme na kuwa na ziada ya umeme wa wastani wa megawati 325.
- Kukamilika kwa miradi ya kuzalisha umeme ya Kinyerezi I megawati 150, kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 183, sawa na shilingi bilioni 315.4 na Kinyerezi II megawati 248.22 kwa

gharama ya Dola za Marekani milioni 344, sawa na shilingi bilioni 794.12. Fedha zote hizo zilitolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ujenzi wa miradi umekamilika kwa asilimia 100 mwaka 2016 na mwaka 2018 mtawalia, ambapo jumla ya megawati 398.22 zimeingizwa kwenye Gridi ya Taifa.

- Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), limeendelea kuimarika na kuweza kujiendesha bila kutegemea ruzuku kutoka Serikalini na limeanza kupata faida na kutoa gawio kwa Serikali. Aidha, Shirika limeanza kuunganisha Mikoa ya Lindi, Mtwara, Njombe na Ruvuma katika Gridi ya Taifa ambako kumewezeshwa kusitisha uzalishaji wa umeme kwa kutumia mitambo

TAARIFA MAALUM YA MAFANIKIO YA SEKTA YA NISHATI KWA KIPINDI CHA MWAKA 2015 - 2020



Utandikaji wa nguzo na nyaya za umeme kwa ajili ya uendeshaji wa Reli ya kisasa na Treni ya umeme.

ya mafuta mazito ambayo ilikuwa inaigharimu TANESCO wastani wa shilingi bilioni 15.3 kwa mwaka katika Mikoa hiyo.

- Kuzimwa kwa mitambo ya kuzalisha umeme inayotumia mafuta kwa ujumla kumeiwezesha TANESCO kuokoa matumizi ya shilingi bilioni 118.175 kwa mwaka, zilizokuwa zikitumika kununua mafuta kwa ajili ya kuendesha mitambo hiyo.
- Kuendelea na utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini ambapo hadi kufikia mwezi Julai, 2020 jumla ya vijiji 9,412 vimeunganishwa kutoka 2,018 vilivyokuwa vimeunganishwa mwaka 2015 ikiwa ni sawa na ongezeko la vijiji 7,394. Vijiji 3,448 vilivyobaki vitaunganishiwa umeme kwa mwaka 2020/21.

Katika kipindi hicho, jumla ya shilingi trilioni 2.29 zimetumika ambapo kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 1.78 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 515.71 ni fedha za nje kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

- Kuendelea na ujenzi wa Mradi wa Julius Nyerere Hydro Power Project (JNHPP) megawati 2,115 ambao hadi sasa utekelezaji wake umefikia zaidi ya asilimia 86 ya kazi muhimu kulingana na Mpango Kazi.
- Fedha zilizolipwa kwa Mkandarasi wa ujenzi wa Mradi wa Julius Nyerere ni jumla ya shilingi trilioni 1.38.
- Katika Mradi wa Julius Nyerere, jumla ya wafanyakazi

TAARIFA MAALUM YA MAFANIKIO YA SEKTA YA NISHATI KWA KIPINDI CHA MWAKA 2015 - 2020



Utafiti wa shughuli za mafuta katika kina kirefu cha maji.

wapatao 3,897 wameajiriwa tangu utekelezaji wa Mradi uanze ambapo kati ya wafanyakazi hao, Watanzania ni 3,422 sawa na asilimia 87.81 na wafanyakazi kutoka nje ya nchi ni 475 sawa na asilimia 12.19 ya wafanyakazi wote wa Mradi. Hadi kukamilika kwa Mradi, Watanzania 6,000 wataajiriwa katika shughuli za Mradi.

- Kuendelea na uzalishaji wa vifaa vya kujenga miradi ya umeme nchini na hivyo kusitisha uingizaji wa vifaa vya ujenzi wa miundombinu ya umeme ikiwemo nguzo, transfoma, nyaya na mita za LUKU ndani ya nchi na hivyo kurahisisha upatikanaji wa vifaa hivyo.
- Kuongezeka kwa kiwango cha upatikanaji wau meme (Overall Electricity Access Rate) nchini



Kituo cha kujaza gesi kwenye magari cha Ubungo jijini Dar es Salaam.



Mwonekano wa baadhi ya miundombinu ya umeme katika mradi wa Kinyerezi I Extension (MW 185).

kutoka asilimia 67.8 mwaka 2016 na kufikia asilimia 78.4 mwezi Aprili, 2020.

- Kuunganishiwa umeme kwa wateja wapya 1,360,424 na kufanya jumla ya wateja waliounganishiwa umeme hadi mwezi Julai, 2020 kufikia 2,833,641 ikilinganishwa na wateja 1,473,217 waliokuwepo hadi Juni, 2015 sawa na ongezeko la silimia 92.
- Serikali kupitia TPDC imeendelea kusambaza gesi asilia kwa wateja wa majumbani na viwandani katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Mtwara na Lindi. Hadi kufikia Juni, 2020 zaidi ya nyumba zipatazo 500 zimeunganishwa na miundombinu ya gesi asilia na viwanda zaidi ya 48 vimeunganishwa. Aidha, zaidi ya magari 400 yamefungwa mifumo

TAARIFA MAALUM YA MAFANIKIO YA SEKTA YA NISHATI KWA KIPINDI CHA MWAKA 2015 - 2020



Utafiti wa kijiofizikia katika miradi ya jotoardhi katika mikoa ya Songwe na Mbeya.



Mitambo ya kufua umeme wa gesi ya Kinyerezi II jijini Dar es Salaam (MW 240).

ya matumizi ya gesi asilia ikilinganishwa na magari 60 yaliyokuwa yameunganishwa mwaka 2015.

- Kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia (trunk-lines) yenye urefu wa kilomita 17 yenye uwezo wa kuunganisha zaidi ya wateja 3,000 wa majumbani katika Mkoa wa Mtwara, kilomita 18 yenye uwezo wa kuunganisha zaidi ya wateja 10,000 wa majumbani katika Mkoa wa Dar es Salaam na kilomita 6 yenye uwezo wa kuunganisha viwanda zaidi ya 20 katika Mkoa wa Pwani (Mkuranga).
- Kuendelea na ujenzi wa Mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia (Liquefied Natural Gas – LNG). Mradi huu unalenga kusindika gesi asilia kuwa kimiminika kwa gesi iliyogunduliwa katika eneo la kina kirefu cha Bahari katika Vitalu Na. 1, 2 na 4. Fidia ya jumla ya shilingi bilioni 5.2 imelipwa kwa wananchi 618 kati ya 693 watakaopisha mradi katika eneo la Likong'o – Lindi. Aidha, Serikali inaendelea na taratibu za malipo kwa wananchi waliobaki na pia kuendelea na majadiliano ya Mkataba Hodhi (Host Government Agreement – HGA) na kampuni zitakazotekeleza mradi.
- Kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP). Mradi huu unahusisha ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi lenye urefu wa kilomita 1,443 kutoka Kabale nchini Uganda hadi mkoani Tanga nchini Tanzania. Gharama za mradi zinakadiriwa kufika Dola za Marekani

bilioni 3.5 sawa na takribani shilingi triloni 8. Kazi zilizokamilika ni pamoja na tafti mbalimbali za kijiolojia, kijiofizikia na kijioteknika na kukamilika kwa kazi ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira. Aidha, utwaaaji wa ardhi katika maeneo ya miundombinu wezeshi upo katika hatua za mwisho za kukamilika. Kwas asa kazi inayoendelea ni majadiliano ya mikataba mbalimbali kati ya nchi hodhi na wawekezaji wa mradi huu.

- Kuanza kutumika kwa Bandari ya Tanga mwaka 2016 na ya Mtwara mwaka 2018 kupokea mafuta kumewezesha upatikanaji kwa urahisi wa mafuta kwa maeneo hayo na vilevile kumeiwezesha nchi kuwa na bandari mbadala zinazoweza kutumika kwa dharura na kuwezesha kuongeza ajira. Hivyo kuendelea kuimarika kwa Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja ambao umeongeza uhakika wa upatikanaji wa mafuta nchini na kupunguza gharama za uagizaji.
- Udhhibiti wa uchakachaji wa mafuta umepungua kutoka wastani wa asilimia 19.2 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 4 mwaka 2019.
- Kuongezeka kwa mchango wa gesi asilia katika kuzalisha umeme kutoka asilimia 36 mwaka 2015 hadi asilimia 57 mwaka 2020.
- Kuongezeka kwa ugunduzi zaidi wa gesi asilia kutoka futi za ujazo triloni 55.27 mwaka 2015 na kufikia futi za ujazo triloni 57.54 mwaka 2019 sawa na ongezeko la zaidi ya futi za ujazo triloni 2.27.

PURA yazindua Baraza la Wafanyakazi

Na JANETH MESOMAPYA

Baraza la Wafanyakazi la Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) limezinduliwa rasmi hivi karibuni mjini Bagamoyo kwa lengo la kuboresha uhusiano baina ya wafanyakazi na uongozi wa Mamlaka hiyo ili kuongeza ari na ufanisi kazini.

Uzinduzi huo uliofanyika mnamo Novemba 13, 2020 na kuhudhuriwa na watu mbalimbali wakiwemo viongozi wa serikali, Mwenyekiti wa Bodi, Menejimenti na wafanyakazi wa PURA pamoja na baadhi ya viongozi wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya (TUGHE) kwa ngazi za mkoa na taifa.

Akizungumza kabla ya kuzindua baraza hilo Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa Wizara ya Nishati Raphael Nombo ambaye alimwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Bi. Zena Said, ameeleza kuwa, baraza hilo lina jukumu la kuhakikisha kuna ushirikiano wa kutosha baina ya Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi.

Alisema kwamba ushirikiano huo utasaidia kuwezesha utendaji mzuri wa majukumu ya Mamlaka hiyo ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya taifa.

“Tunafahamu kuwa nia ya serikali katika kuanzisha mabaraza ya wafanyakazi ni kuwa na chombo kinachohakikisha kuwa haki na wajibu wa mwajiri na mtumishi vinapewa kipaumbele katika utekelezaji wa majukumu,” alieleza.

Aliongeza kuwa baraza ni chombo chenye



Kutoka kulia ni Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi ambaye pia ni Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa PURA, Charles Sangweni, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa Wizara ya Nishati Raphael Nombo, Katibu wa Baraza la Wafanyakazi PURA, Deborah Mgombela na Katibu Mkuu wa TUGHE taifa, Heri Mkunda.

kuangalia maslahi ya pande zote mbili kwa manufaa ya taasisi na taifa kwa ujumla pamoja na kuibua hoja mbalimbali za kuongeza mafanikio ya taasisi.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa PURA, Mhandisi Charles Sangweni alieleza kuwa kuwepo kwa baraza hilo la wafanyakazi wa Mamlaka hiyo kutaongeza kasi, ufanisi, na weledi katika kutekeleza majukumu yao kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Petroli ya mwaka 2015.

Alibainisha kuwa mabaraza ya wafanyakazi huanzishwa kisheria kwa madhumuni ya kuishauri serikali katika ngazi za idara zinazojitegemea, taasisi na wizara kuhusu usimamizi wa kazi na rasilimaliwatu, utekelezaji wa majukumu na kulinda haki na wajibu wa waajiri na wafanyakazi.

Aliongeza kwamba mabaraza hayo pia huanzishwa ili kutia

INAENDELEA UK.

17



Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa PURA Charles Sangweni, akisoma hotuba kwenye uzinduzi wa Baraza la Wafanyakazi PURA.

PURA yazindua Baraza la Wafanyakazi

INATOKA UK.

16

ushauri kuhusu kujenga hali bora za kazi, maslahi ya wafanyakazi na kusimamia haki na ustawi katika sehemu za kazi.

“Wajibu wa mabaraza haya kama vyombo vya ushauri na usimamizi ni kuhakikisha kuwa waajiri

na watumishi wanatambua wajibu na haki zao, pia wanazingatia maadili ya utumishi wao ili kuleta matokeo ya utendaji kazi wenye tija, staha na upendo,” alifafanua.

Aliwataka viongozi na wawakilishi wa baraza hilo kufanya kazi kwa bidii huku wakimtanguliza Mwenyezi Mungu na wakizingatia nidhamu,

uwajibikaji na uadilifu.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya PURA Profesa Gasper Mhinzi aliipongeza Mamlaka kwa hatua hiyo muhimu ya kuzindua Baraza la Wafanyakazi na kuwatakia heri katika utendaji kazi wake.

Baraza hilo jipya la wafanyakazi PURA lina wajumbe wapatao 34

likihusisha wajumbe kutoka Menejimenti ya PURA ambao ni 13, na wajumbe wa kuchaguliwa na wafanyakazi kutoka kila idara ambao ni nane.

Wengine ni wajumbe wa Halmashauri ya tawi la TUGHE ambao wako 11, mjumbe mmoja kutoka TUGHE mkoa na mjumbe mmoja kutoka Baraza Kuu la Wafanyakazi Serikalini.



Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa Wizara ya Nishati Raphael Nombo akisoma hotuba ya mgeni rasmi kwenye uzinduzi wa Baraza la Wafanyakazi PURA.



Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa Wizara ya Nishati Raphael Nombo (kushoto) akiipeana mkono na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa PURA Charles Sangweni baada ya kuzindua Baraza la Wafanyakazi PURA.



Wafanyakazi wa PURA na Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wakipitia nyaraka mbalimbali katika uzinduzi wa Baraza la Wafanyakazi PURA.

Picha za matukio kwenye uzinduzi wa Baraza la Wafanyakazi PURA, lililofanyika Novemba 13, 2020 Bagamoyo



Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi na Kaimu Mkurugenzi Mkuu PURA (aliyesimama) Charles Sangweni, akisoma hotuba ya uzinduzi wa Baraza la Wafanyakazi PURA kwa Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa Wizara ya Nishati Raphael Nombo (wa pili kulia). Anayewafuatia ni Katibu wa Baraza la Wafanyakazi PURA, Deborah Mgombela na Katibu Mkuu wa TUGHE taifa, Heri Mkunda.



Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa Wizara ya Nishati Raphael Nombo (katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi PURA Profesa Gasper Mhinzi (kulia kwake), Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa PURA Charles Sangweni (kushoto kwake), viongozi na wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi PURA na wawakilishi kutoka Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya (TUGHE) ngazi ya taifa, baada ya kuzindua Baraza la Wafanyakazi la PURA.



Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa Wizara ya Nishati Raphael Nombo akizungumza jambo na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa PURA Charles Sangweni (kulia) pamoja na na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi PURA Profesa Gasper Mhinzi (katikati).

JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI



Fika Ofisi ya Mawasiliano,
Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au
Wasiliana nasi kwa **simu namba** +255-26-2322018
Nukushi +255-26-2320148

www.nishati.go.tz

[Wizara ya Nishati](https://www.facebook.com/Wizara.ya.Nishati)

[@Nishati2017](https://twitter.com/Nishati2017)

[wizara_ya_nishati_tanzania](https://www.instagram.com/wizara_ya_nishati_tanzania)

[Wizara ya Nishati](https://www.youtube.com/Wizara.ya.Nishati)